


# MBINGUNI NA JEHANAMU

Na mchungaji Park Yong Gyu

www.DivineRevelations.info/SWAHILI

Mnamo mwaka wa 1987, mchungaji Park alifariki kutokana na ugonjwa wa shinikizo la damu. Lakini kwa neema ya Mungu, maisha yake yaliongezwa kwa miaka mingine ishirini. Lakini kwa miaka minne ya kwanza kati ya hii miaka ishirini hakuweza kuongea kutokana na hali yake. Alikuwa na miaka takribani hamsini alipofufuliwa. Katika kifo chake Bwana alimuonyesha Mbinguni na Jehanamu.



Nataka ufahamu kwamba, ukiwa mwenye kiburi na majivuno utajiletea laana. Nilikuwa na kanisa kubwa mno lenye washirika elfu tano lakini Mungu alinichapa kichapo kutokana na kiburi changu.Sasa namuogopa Mungu.

Nilikuwa na mali ya takribani dola million mia moja hamsini. Nilikuwa na magari matano ya kifahari .Lakini baada ya mkasa wa kufa na kufufuliwa kwangu nilipeana vyote. Tafadhali kumbuka kwamba wokovu hauwezi kupatikana kupitia kwa mali uliyonayo ila ni kwa imani pekee. Na sasa nawasihi mashemasi wote, wazee wa kanisa na viongozi wengine wa makanisa kuwatumikia wachungaji wao kwa mioyo yao yote.

Mnamo Desemba kumi na tisa mwaka wa 1987, baada ya kumaliza kula chakula cha mchana nilipokuwa napumzika, nilianza kuhisi uchungu mkubwa mno, ulikuwa uchungu nisioweza kuustahimili nami nilihisi kana kwamba nitakufa. Kisha nikapoteza fahamu. Niliamka miezi minne baadaye nikiwa katika hali mbaya sana tena mahututi, kisha Daktari akaniambia kwamba nitakufa.



Sehemu zote za mwili wangu zilikunjana vibaya kutokana na kupooza kwanga. Hata jamii yangu haikuwaruhusu washirika wa kanisa langu kunitembela kutokana na jinsi mwili na hali yangu ilivyokuwa mbaya. Mwishowe nikafariki.

Nilipofariki, niliwaona watu wawili wakiingia chumbani mwangu. Lakini watu hawa waliingia chumbani mwangu kupitia ukuta. Nikapiga ukulele nikauliza, “kina nani nyinyi? Nyumba yangu itaporomoka mkiingia jinsi mlivyofanya.” Mmoja wao akasema, “sisi tu malaika tulioshuka kutoka  mbinguni, tumetoka katika ufalme wa Mungu”. Mwangaza mkali ulimulika kutoka kwa Malaika wale.

Malaika aliyekuwa mkono wangu wa kulia akajitambulisha hivi, “mimi humtekelezea Yesu kazi za ujumbe katika ufalme wake. Yesu aliniita akaniamauru nishuke duniani nije nikuchukue Mbinguni. Wewe umefariki lakini kwa vile jamii yako inalia kwa huzuni sana, Yesu anataka kukuongezea muda kidogo wa ziada wa kuishi duniani. Lakini kwa sasa anataka kukuonyesha Mbinguni na Jehanamu. Yeye atakuonyesha nawe utawashuhudia watu wa ulimwengu. Na idadi ya wale wangetokomea Jehanamu itapunguka, nayo idadi ya wale watakao enda Mbinguni itaongezeka kupitia kwa ushuhuda wako. Huu ndio utakuwa ujumbe wako.

“Mungu ametuagiza tukuambie usichelewe kwani ukichelewa basi hautaweza kuzuru Mbinguni na Jehanamu”.

Kisha malaika aliyekuwa mkono wangu kulia akasema, “tangu pale ulipozaliwa hadi wakati ulipoaga dunia, nimekuwa nawe”. Mimi sikuelewa alichomaanisha malaika huyo lakini sasa nimefahamu alikuwa malaika wangu mlinzi. Basi nikasema, “siwezi kwenda! Nami sitaenda! Mimi ni mchungaji! Siwezi kukutana na Bwana katika hali hii niliyonayo.Nataka tukutane naye nikiwa mtu mwenye afya. Mimi pengine nitapokea makemeo mengi kuliko pongezi kutoka kwa Bwana. Mimi ni mtu mwenye kiburi na majivuno na sasa nimelaaniwa tena ni mgonjwa. Nitawezaje kuingia mbinguni? naogopa sana.Tafadhali rudini mbinguni mumsihi Bwana aniponye .Kisha mtarudi mnichukue mbinguni kupitia kwa ndoto.Tafadhali nawasihi mniombee msamaha kwa Bwana kwa niaba yangu”.



Lakini malaika hawakuwa wakiisikia hoja yangu. Wakanivua nguo zangu kisha wakasema zilikuwa chafu mno na hazifai kuvaliwa mbinguni. Nao wakanivisha vazi jeupe.



Wakanishika mikono yangu nasi tukapaa moja kwa moja hadi mbinguni. Tulipaa mawinguni na nilipotazama chini nikaona dunia ilikuwa ndogo. Wakaniacha niende karibu na njia ya dhahabu isiyokuwa na mwisho. Nikaona mwangaza mkali mno. Nikauliza, “mwangaza huu watoka wapi?” nao wakanijibu kwamba watoka mbinguni.

Nikawaza, “Lo ni pakubwa mahali hapa!” Nikaona kikundi cha watu waliovalia mavazi meupe wakipaa mbele yetu. “Kina nani wale?” nikauliza. Malaika akajibu. “Hao ni wale waliomtumuikia Yesu kwa kutii na kufuata kuongozwa na Roho mtakatifu. Miili yao imekufa duniani. Sasa nafsi zao zinaelekea mbinguni”. Huyo malaika mwingine akaendelea. “Kuna malango kumi na mbili mbinguni. Wakati nafsi iliyookoka inapowasili mbinguni, ni sharti iingie kupitia moja wapo ya malango

haya.” Tulikuwa tumesimama katika lango la kusini lakini lilikuwa limefungwa. Tulipokuwa tunangoja nikamuuliza malaika. “Mbona lango halifunguki?” naye akanijibu “ni kwasababu hauuimbi wimbo wa kuabudu wa mbinguni.” Nikamuuliza malaika, “nilikuwa na kiburi tena mwenye majivuno na ndio sababu ya mimi kulaaniwa na ugonjwa, ikiwa mimi sio mkakamavu wa kuziimba nyimbo za kuabudu za duniani, nitawezaje kuziimba nyimbo za kuabudu za hapa mbinguni nami sijawahi kuzisikia?”

Naye malaika akanijibu, “ulivyosema ni kweli lakini sharti ujitayarishe kuabudu. Wewe ni mtu mwenye majivuno lakini jitayarishe kuimba.” Nao malaika wakaanza kuimba na walipokuwa wakiimba nami pia nikaanza kuimba nao. Kuimba kule kukawa kawaida kwangu, basi tukaingia ndani.

Eneo la mbinguni lilikuwa zuri ajabu hata siwezi kueleza kwa maneno ya humu duniani. Nami nikasema “ Bwana! Asante Sana! Japo nilikuwa mwenye kiburi na majivuno na aliyelaaniwa kwa ugonjwa, umenileta mbinguni kunionyesha sehemu zake.”

Kisha nikasikia sauti ya Mungu, “mchungaji wangu mpendwa PARK Yong GYU”, nakukaribisha. Umefanya safari ndefu sana kuja hapa.”

Sauti yake ilijawa na upendo tena ilikuwa nyororo sana.

Nami nakamjibu huku nikilia kwa machozi, “Bwana…” wale malaika mara moja wakasema, “umekuwa mchungaji kwa miaka ishirini, kwani hauyajui maandiko”, mbinguni hakuna machozi. Tafadhali usilie hapa” sikuweza hata kulia. (Ufunuo 21:4)

Bwana akaniuliza maswali matano:



1. Uliutimia wakati wako kiasi gani kuisoma bibilia?
2. Ulitoa sadaka kiasi gani?
3. Mara ngapi umeeneza injili kwa watu?
4. Je? Ulitoa zaka ipasavyo?
5. Uliutumia mda wako kiasi gani katika maombi?

Nikashindwa kulijibu swali la tano. Naye Bwana akanikemea kwa ajili ya swali hilo la tano.

“Baada ya kuwa mchungaji wa kanisa kubwa ukawa mvivu wa maombi. Kuwa na shughuli nyingi sio udhuru kwangu!” ilinibidi nitubu kuhusu hili jambo baadaye. “Malaika hao watakuonyesha sehemu nyingi hapa mbinguni na pia jehanamu. Tazama jinsi utakavyo. Nawe utaondoka baada ya kuzishuhudia sehemu tofaui za mbinguni na pia jehanamu.” Lakini Bwana hakuniruhusu niutazame uso wake.

Malaiaka wakanipeleka sehemu tatu tofauti za mbinguni.



Sehemu ya kwanza, niliwaona watoto wadogo wakiishi pamoja. Sehemu ya pili paliishi watu wazima. Sehemu ya tatu palikuwa na nafsi ambazo ziliingia mbinguni chupuchupu. Hata kama waliwahi kuingia mbinguni, wao waliingia kwa njia ya aibu.

Watu wengi waliniuliza umri wa wale watoto. Walikuwa kana kwamba waliokuwa shule ya chekechea. Kila mtoto alikuwa na malaika wake mtoto wa kuandamana naye.

Mbinguni nafsi nyingi zitakuwa na makao yao binafsi. (Yohana 14:2)

Lakini kuna wale amabao hawakuwa na makao. Hii nitafafanua baadaye. Tena wale watoto hawakuwa na makao yao. Nami nikauliza, “ hawa watoto pia ni nafsi ,mbona hawana makao?”

Malaika akanijibu, “hata jinsi duniani watu huhitaji  vifaa vya kujengea nyumba , hali ni hiyo hiyo hapa mbinguni. Wakati mtu anapoihudumia kanisa na watu wengine kwa utiifu katika Bwana, haya matendo mema ndio huwa vifaa vya kumjengea mtu nyumba hapa mbinguni”. Wakati vifaa hivi vinapotolewa basi malaika waliopewa jukumu la kumjengea mtu nyumba huanza kazi ya ujenzi hapa mbinguni. Kwa vile hawa watoto walikuwa chini ya umri wa kuwajibika, basi hawangeweza kujilimbikizia au kupata vifaa vya kujijengea nyumba hapa mbinguni. Kwa ufupi, hawakuwa na muda wala nafasi ya kujikusanyia vifaa vya kujengea nyumba na ndio maana hawana makao.”

Nami nikanedelea kuuliza maswali, “nitafanyaje nikiwa duniani ili nipate vifaa  vingi vya kuijengea nyumba yangu hapa mbinguni?” nao wakanijibu, “kuna vitu saba impasavyo mtu kuvifanya ili kupata na kujilimbikzia  vifaa vya kujengea nyumba.”



1. Kwanza ni malimbikizi yao ya sifa na kumuabudu Mungu.
2. Pili ni wakati wautumiao kuisoma bibilia.
3. Tatu ni wakati wautumiao kuomba.
4. Nne ni wakati wautumiao kueneza injili.
5. Tano ni sadaka wazitoazo kwa Bwana.
6. Sita ni utiifu katika kutoa zaka.
7. Saba na ya mwisho ni ule wakati mtu autumiao kuitumikia kanisa kwa njia yoyote ile.

Haya ndiyo matendo ya utiifu yamwezeshayo mtu kukusanya vifaa vya kujengea nyumba zao huko mbinguni.

Palikuwa na watu wengi amabao hawakuwa na nyumba huko mbinguni .Wengi wa wale ambao hawakuwa na makao huko mbinguni ni wachungaji, ,mashemasi na hata wazee wa kanisa. Nami nikauliza kwa udadisi, “Basi hawa watoto wanaishi wapi?”



Malaika akanijibu, “wao huishi hapa”. Nilipotazama hapa na pale, niliona wamekusanyika pote kwenye bustani la maua. Bustani hilo la maua lilikuwa zuri ajabu na lilikuwa na harufu nzuri sana isiyopatikana humu duniani.

Eneo lile lilikuwa nzuri kushinda jinsi ninavyoweza kueleza kwa maneno yangu binafsi.

Mahali pa pili palikuwa na watu wazima waliokuwa waaminifu. Kuna tofauti kati ya wokovu na kutuzwa. Mahali hapo palikuwa na nyumba nyingi sana. Nazo nyumba hizo zilijengwa kwa vito vizuri sana pamoja na mawe ya thamani ambayo ni adimu mno. Baadhi ya makao yale yalikuwa marefu sana kama zile nyumba ndefu za gorofa humu duniani. Wale watu amabo walimtumikia Bwana kwa uaminifu wakiwa humu duniani walikuwa na nyumba zilizojengwa kwa vito vizuri pamoja na mawe ya thamani ambayo ni nadra sana.



Katika mahali hapa, watu walionekana kana kwamba wana umri wa miaka ishirini hadi thelathini. Hapakuwa na wake au waume kulingana na jinsia. Hapakuwa na watu wagonjwa, wazee au viwete.

Niliwahi kumjua mzee mmoja aitwaye Oh Im Myung. Alifariki akiwa na miaka sitini na tano. Alikuwa mtu mfupi mno, urefu wake ulikuwa kama wa watoto wa darasa la pili hivi. Aliteseka sana kutokana na ugonjwa wa nyongea lakini yeye alibobea sana katika mambo ya bibilia.Alikuwa ameaandika mafafanuzi mengi sana ya bibilia .Nilikutana naye mbinguni naye alikuwa buheri wa afya . Mbinguni ni mahali pazuri sana. Nina matarajio mengi sana. Tafadhali aminini yale ninayowaambia wapendwa wenzangu.

Mahali pa tatu palikuwa na wale ambao waliokolewa kwa njia ya aibu. (Wakorintho 3:15). Kijiji hiki kilikuwa kikubwa sana, na kilikuwa ni kikubwa zaidi ya mahali pale pa pili ambapo nyumba zilijengwa kwa vito vya thamani na mawe ya thamani yaliyo nadra.

Nilifika mahali hapa kwa kasi sana nikiwa nimeabiri gari la farasi wa dhahabu.Palikuwa mbali sana na sehemu nzuri za mbinguni ambazo niliziona hapo awali.

Nikawauliza wale malaika, “naona jangwa kubwa mno na viwanja, mbona sioni nyumba?” malaika akanijibu, “kile unachotazama ni makao”.



Niliona nyumba kubwa sana tena pana ambazo zilinikumbusha nyumba za kuku au mabohari. Makayo haya hayakuwa mazuri bali yalikuwa chakavu. Kijiji hiki na nyumba zile zilikuwa za zile nafsi ambazo ziliokolewa kwa aibu. Palikuwa na nyumba kubwa tena nyingi sana ambazo ziliikuwa chakavu. Mji huu ni mkubwa mara kadhaa zaidi ya pahali ambapo nafsi zilizotuzwa zinapokaa.

Malaika akasema, “ je ? Waona nyumba mbili kubwa zilizoko kushoto na kulia kwako?” nami nikamjibu “naam nimeziona”.

Malaika akasema kwamba alitaka kunionyesha nyumba hizo mbili haswa.Akasema “nyumba iliyopo mkono wa kulia ni ya wale waliokuwa wachungaji duniani. Nayo iliyoko mkono wa kushoto ni za wazee wa kanisa.

Tulipofika mbele ya nyumba zile nikaona zilikuwa kubwa ajabu. Nami nikabaki kinywa wazi!. Tulipofungua mlango na kuingia matarajio yangu yalikuwa ni kama tunaingia nyumba ya kuku.

Badala  ya kuona maelfu ya kuku  mahali pale, niliona nafsi . Malaika akanishauri nitazame kwa makini kwani nitaweza kuwatambua wachungaji maarufu katika historia. Ilikuwa ukweli. Niliwatambua wachungaji wengi katika historia. Niliwahi kumuona mchungaji mmoja haswa,nami nikamuuliza malaika, “namjua mchungaji huyo amabaye ni mkorea, najua jinsi alivyo kuwa maarufu na ile kazi amemfanyia  Bwana . Mbona yuko hapa? Sielewi!”



Nikauliza kwa udadisi, “hii ilifanyikaje? Mbona hakuwa na vifaa vya kumjengea nyumba?” Malaika akanijibu, “wakati alipokuwa akifanya kazi yake ya uchungaji, alipenda kusifiwa sana na watu. Alipenda kuheshimiwa sana. Pia alipenda kutumikiwa. Hakuwa na kujitolea wala utumishi kwa upande wake.” Huyu mchungaji aliheshimika sana Korea tena alikuwa bingwa mkubwa katika historia ya kanisa la Korea. Lakini hakutunukiwa chochote!

Enyi wachungaji mlio huko nje, tafadhali sikieni. Inawapasa kuwaongoza watu zaidi ya ile ibada ya jumapili kanisani. Sharti uwatembelee majumbani mwao. Sharti uwatunze masikini, viwete na wazee.

Wachungaji waliotumikia bila ya kujitolea maisha yao, ambao walipenda kutukuzwa hawana zawadi yoyote mbinguni.

Baada ya Mimi kuvishuhudia vitu hivi mbinguni na kurudi hapa ulimwenguni, nilipena vyote nilivyokuwa navyo vikiwemo magari yangu ya kifahari. Maisha yetu ni ya muda mfupi tu. Kataika bibilia maisha ya mwanadamu ni takribani miaka sabini hadi themanini. Lakini ni Mungu pekee ajuaye atakapofariki mtu. Yeyote aweza kufa kabla ya miaka sabini au themanini. Niliamua kupena vyote nilivykuwa navyo hata nguo zangu.

Wale niliowaona wamepokea wokovu kwa aibu walikuwa wachungaji,wazee wa kanisa,mashemasi na hata waumini wa kawaida.Palikuwa na umati wa wazee wa kanisa na mashemasi katika nyumba hizi chakavu. Lakini hata hivyo, ni bora kuliko jehanamu. Licha ya hayo, mtu gani angependa kuingia mbinguni kwa njia hii?. Mimi sitaishia mahali pale pa aibu. Hata nguo zao zilikuwa chakavu.

Ni masharti yapi yampasayo mkristu kufuata ili apate makao yanayopendeza mbinguni? Kwanza ni sharti tueneze injili kwa watu wengi kabisa iwezekanavyo. Nasi tutaieneza injili vipi? Malaika akaniambia, “hebu dhania kwamba pana mtu asiyekuwa muumini au asiyeokoka ambaye hamjui Bwana. Wakati uamuapo kumuenezea injili mtu huyo, basi vifaa vya kukujengea nyumba mbinguni vitatolewa. Unapozizdi kuombea wokovu wao, basi vifaa zaidi hutolewa kwa ajili yako. Lazima uendelee kuwatazama na kuwaanagali, kuwatembelea na kuwaeleza kuhusu injili. Hii itakuongezea vifaa zaidi kwa ujenzi wa nyumba yako.



Ikiwa mtu atasema hawezi fika kanisani kwa sababu hana nguo nzuri basi lazima umpatie. Ikiwa mtu atasema hana miwani ya kusomea, basi wewe mpe. Ni sharti umpe mtu Yule chochote uwezacho ili yeye aweze kuongozwa kwa Bwana.


Wale waishio kwenye nyumba zilizo nzuri zaidi ni wale ambao wameeneza injili kwa wingi.

Kisha malaika akanisindikiza mahali ambapo watakatifu waliishi katika makao mazuri. Hapa ndipo walioeneza injili kwa wingi waliishi. Ilikuwa ni kama sehemu ya hali ya juu huko mbinguni.

Katika historia ya ukristo kuna watu wanne ambao wana moja wapo za nyumba kubwa sana tena za kupendeza sana. Malaika akanionyesha nyumba ya mwinjilisti wa kimarekani D.L Moody, mchungaji wa uingereza John Wesley, mwinjilisti wa kiitaliano na mwinjilisti wa kikorea mchungaji Choi Guu Nung. Hawa wane wana mmoja wapo za nyumba kubwa sana mbinguni. Wanne hawa waliyatumia maisha yao yote kuieneza injili kwa watu hata mpaka wakati wa kufa kwao.

Katika Waumini wa kikorea, palikuwa na muumini wa kawaida alieykuwa na jumba kubwa. Huyu muumini alijenga makanisa mengi. Alikuwa amepeana magunia elfu tatu ya mchele kwa masikini. Kwa kisiri aliwasiadia maelfu ya wachungaji na viongozi wa kanisa katika hali ya kifedha. Yeye pia aliwasaidia wanafunzi waliokuwa wakisomea thiologia na waliokuwa katika vyuo vya masomo ya bibilia. Alimchukua mchungaji wa miaka sitini na tano nyumbani mwake naye akamtunza vyema.

Mchungaji huyu alikuwa amefukuzwa kutoka kanisa lake.



Nikasikia malaika akisema, “kuna vifaa vimewasili!”. Nikamhoji malaika aliyekuwa kulia kwangu kuhusu vifaa hivi vilivyowasili, naye akaniambia. vifaa hivi ni vya shemasi wa kike kutoka kanisa dogo. Kwa kweli yeye hupokea vifaa kila siku. Ingawa yeye ni masikini, yeye huja mapema kwa ibada ya asubuhi kila siku. Yeye huawaombea washirika themanini na saba kila siku. Amalizapo kusali yeye huisafisha kanisa.

Nikasikia malaika mwingine akisema kwa sauti, “utoaji maalum umeasili, bintiye shemasi wa kike ametoa pesa kidogo amabzo ndizo zote alizokuwa nazo na kumpa mama yake. Lakini shemasi yule hakuzitumia kwa ajili yake binafsi bali alimnunulia mchungaji mayai matano na jozi mbili za soksi”. Ingawa itaonekana ni sadaka kidodgo yeye alipeana vytoe alivyokuwa navyo siku hiyo.



Hivi vikawa vifaa maalum vya kuijengea nyumba yake mbinguni.

Pili, wale ambao pia wana nyumba kubwa ni wale waliojenga makanisa au majumba mengine kwa ajili ya ufalme wa Mungu wakitumia rasilmali zao.

Mbinguni pia nilikutana na mzee aitwaye Choi, kati ya wazee wa kikorea na mashemasi walioko mbinguni, yeye alikuwa na nyumba nzuri zaidi. Nyumba yake ilikuwa ndefu kuliko jumba ndefu zaidi nchini Korea. Choi alijenga makanisa mengi nchini Korea kwa kutumia mali yake.

Nikamuuliza malaika, “na nyumba yangu je?, bado iko katika hali ya kujengwa?”  Naye malaika akanijibu, “ndio”. Nikamsishi niione nyumba yangu lakini wakaniambia haikuruhusiwa. Nilizizdi kumsishi na baada ya kusisitiza kwangu , wale malaika wakanijibu kwmaba Bwana sasa ataruhusu.

Tukaingia kwenye gari livutwalo na farasi na tukasafiri mbali sana mpaka mahali pengine. Nilijawa na matarajio. Nikauliza, “ nyumba yangu I wapi?” malaika akanijibu, “iko pale”. Lakini ikaonekana ni kana kwamba mahali pale palikuwa ni msingi tu tayari kwa kujengwa.

Nami nikauliza kwa sauti, “mbona mkanifanyia hivi? Hii itawezekanaje? Itakuaje nyumba yangu I katika eneo linalokuwa?”  Nikiwa mnusurika wa vita vya kikorea , niliuza nyumba yangu ya kipekee ili nijenge kanisa. Hili kanisa mwishowe lilikuwa hadi likawa na washirika elfu tano. Niliandiaka vitabu vingi kwa muelekezoa wa Roho mtakatifu. Kitabu kimoja kikauza sana. Kupitia kwa mapato ya kitabu hicho nikajenga shule ya kikristo. Shule hiyo ikawawazaa wachungaji mia mbili arubaini. Katika hatamu yangu kama kiongozi, nilipeana udhamani kwa zaidi ya watoto mia nne waliokuwa masikini. Nimewajengea nyumba wajane ili waishi mle. Hii yote iligharimu pesa nyingi sana. Saa mbona mambo yakawa hivi ? kwa nini nyumba yangu imo eneo ambalo bado linakua? nimeghadhibika sana”.

Malaika akajibu kwa ukali, “wewe haufai kamwe kuishi kwenye nyumba nzuri mbinguni kwani umeheshimiwa na watu idadi isiyoweza hesabika”. “Kila wakatai ulipojenga au kufanya jambo nzuri, ulisifiwa na watu. Hata vyombo vya habari huko duniani vilikusifu. Kwa ajili ya hii matendo yako yote yalikuwa ni bure”. (Mathayo 6:1)

Nikaitazama nyumba yangu katika eneo lile ambalo ndilo mwanzo linajengwa. Lilikuwa liko kati ya nyumba zingine tatu. Lilikuwa na gorofa tatu pekee. Nyumba yangu Ilikuwa na vyumba vingi vidogo katika orofa mbili za kwanza. Nikamuuliza malaika. “mbona nina vyumba vidogo hivyo?” naye malaika akanijibu” vyumba hivyo ni vya wana na mabinti wako.”   “Nina watoto wane pekee” nami nikamjibu. Malaika akanifafanulia “la sio za watoto wa kidunia bali ni za wale amabao uliwainjilisha na wakaokoka”. Nikapendezwa sana nikauliza “li wapi chumba changu kikuu cha kulala?.” Malaika akasema ki juu ya paa. Hii ikanitatiza sana. Chumba changu hakikuwa kimemaliza kujengwa. Kwa sauti ya kukasirika nikasema, “ni ndogo sana! Mbona ni vigumu kuimaliza?”. Malaika akajibu, “wewe bado hujafa, hatuwezi kuimaliza nyumba yako au vyumba vyake kwasasbabu hatujui kama vifaa zaidi vitatolewa. Umeelewa?”



Tulipoingia chumbani mwangu, nikaona vyeti vikining'inia ukutani , basi nikaenda kuvisoma. Cheti cha kwanza kilieleza nilipokuwa na miaka kumi na minane nikiishi kwenye nyumba ya watoto mayatima. Siku ya krismasi, nilikuwa narudi kutoka ibada ya asubuhi kanisani nikamuona mzee Fulani akitetemeka pale barabarani. Nikalitoa koti langu nikampa. Tendo hilo likanipa tuzo mbinguni. Cheti cha pili kilieleza tukio lilo hilo lakini ilikuwa kwa ajili ya mkate niliomnunulia mzee huyo kutumia pesa zangu kidogo nilizokuwa nazo. Zile pesa sio muhimu. Kitendo lazima kaindamane na imani au kujitolea kwa kweli. Kiasi cha pesa au zile dola hazikuwa muhimu.





Tuliondoka mahali pale tukarudi. Tulipokuwa njiani mmoja wa wale malaika akaniuliza , " je umesononeka? Nitakuambia jinsi ya kujengewa nyumba ya kupendeza". "Bwana alisema urudipo duniani, lazima uwaambie watu kuhusu mbinguni na jehanamu jinsi ulivyzishuhudia. Pili Bwana anataka ujenge mahali pa kuwakusanya wachungaji wazee wa kike na mashemasi ambao hawana makao au pa kwenda.Ikiwa utafanya hivi kwa uaminifu basi utakuwa na nyumba nzuri.

## JEHANAMU

Wale Malaika wawili wakanipeleka jehanamu. Wakasema, "sasa utazuru jehanamu. Wewe haufahamu ukubwa wa jehanamu." Nilizizdi kusema kwa sauti "nipakubwa sana! Niapakubwa sana!" . Hapa ndipo mahali nafsi zizlizolaaaniwa milele huwekwa. Ilihisika kana kwamba jehanamu ni kubwa sana mara elfu kuliko dunia. Nusu ya jehanamu ilikuwa nyekundu na nusu ingine ilikuwa nyeusi tititi. Nikawauliza malaika "mbona sehemu hii ni nyekundu?" nao wakanijibu. "Kwani hufahamu, ni madini ya kiberiti yanayoungua. Nusu ya pili ni giza. Watu wafanyao dhambi na kuishia hapa watateswa toka pande zote". Kuna makanisa mengi sana duniani na nyingi yazo zimejawa na watu wengi amabao wengi wao sio wakristu wa kweli. Wao ni wale wajao kanisani tu. Kanisa za kweli zitaamini kwa ukweli kwamba kuna mbingu na pia jehanamu.




Maisha ya wakristu wengi yana machafuko mengi kwani hawaamini kwa dhati kuwa kuna mbinguni na jehanamu.

Nafsi moja iingiapo mbinguni, nafsi elfu moja zilizolaaniwa huingia jehanamu. Uwiano wa wale waingiao mbingunia na wale waingia jehanamu ni moj kwa elfu. (Mathayo 7:14)

Mimi ni mchungaji wa kiprisbiteriani aliye fahamika sana. Nimehitimu kutoka chuo kikubwa cha masomo ya kibilia nchini Korea. Sikuamini hivi visa kuhusu jehanamu na mbinguni. Lakini sasa mimi ni Yule aandikaye mashuhudio yangu ili kuwashuhudia wengine.

Ingawa waweza amini wewe ni mkrsito, ikiwa unayaishi maisha kulingana na matakwa ya mapepo basi utaishia jehanamu.

Mahali pa kwanza nilipopaona ni mahali pa madini ya kiberiti yanayoungua.wewe huwezi hata kudariria jinsi mioto ya jehanamu ilivyo. Hakuna awezaye kuusthimili moto huo.

Watu waliojehanamu hutamka mambo matatu. Kwanza pana joto jingi na wanahisi kufa (luka 16:24)

Pili, wana kiu kingi na wanahisi kufa. Tatu utasikia wengi wakiitisha maji (zecheria 9:11)



Na mateso haya ni ya milelel!. Watu wengi husema tuko uhuru katika Kristo nao huishi maisha yao watakavyo. Nikamuuliza malaika, “wale waliomo humu wamefanya nini?” wakanijibu . “kikundi cha kwanza ni wasio waumini, wale ambao hawajaziinjilisha jamii zao lazima watubu”. Malaika akaendelea, “kundi la tatu ni la wale waliomwamini Yesu lakini hawakutubu dhambi zao”. Ni lazima tutubu dhambi zetu na kumkiri Yesu ni Bwana. Tusitende dhambi. Kunyamaza tu sio kutubu. Kwa mioyo iliyopondeka yatupasa kutubu.

# WAKRISTU JEHANAMU

Kisha nikawaona wachungaji wengi, wazee wa kanisa na mashemasi wakiwa jehanamu. Nikawauliza malaika. “Nawafahamu watu hawa, walimtumikia Bwana kwa uaminifu wakiwa duniani. Walifariki wakati mwingine iliopita na sote tulidhani wako mbinguni na Mungu, lakini sasa nawaona wote jehanamu tena wanalia kwamba moto ni mkali sana, mbona wako hapa?” palikuwa na wachungaji wengi, wazee wa kanisa,mashemasi na waumini wa kawaida wengi .

Malaika akajibu, “mchungaji Park Yong GYUU mtu anaweza onekana kuwa mfuasi wa kweli wa Yesu kutoka nje lakini Mungu ndiye aijuaye roho ya mtu na yale yaliyomo ndani mwake”.

Hawakuichukua jumapili kuwa siku takatifu. Walipenda shughuli za kutafuta pesa jumapili. (Jer 17:27)



Mashemasi wengi na wazee wa kanisa waliyashutumu mahubiri ya wachungaji wao .(zaburi105:15) (hesabu 12:8-9)

Hawakutoa zaka ipasavyo. (Malachi 3:9) hawakuomba. Hawakueneza injili kwa watu kamwe . (Ezekiel 33:6). Wengi wa wazee hawa na mashemasi waliwasumbua wachungaji wao na kuyapinga mamlaka yao.

Waliyatatiza majukumu na shughuli za wachungaji . Wakiwa vitandani mwao karibu kufa. Walidhani kuwa walikuwa wamefanya kazi nzuri hapa duniani, kwa hiyo hawakutubu dhambi zao. Hii ndio sababu walitupwa kwenye mioto ya jehanamu.



Kisha nikaona mfalme na mwana wa mfalme waliowatesa wakristo nchini Korea. Mfalme huyu na huyo mwana wa mfalme waliwakata vichwa wengi wa waumini wa kwanza nchini korea. Waliwekwa katikati mwa jehanamu ambapo moto ulikuwa mkali zaidi kuliko sehemu zingine zote.

Niliwaona Hitler,Stalin, Mae Zedong na mhubiri mashuhuri kutoka Korea kaskazini aitwaye mchungaji Kang, shujaa Fulani wa kijapanisi na wengine wengi.

Kisha tukawasili mahali penye giza totoro hadi hungeweza kuona mahali ukanyagapo. Nikapiga kelele, “malaika! kuna giza jingi sana, mimi nitaonaje chochote?” malaika akanipapasa begani mwnagu akasema “ngojea kidogo tu”.

Baada ya muda kidogo, niliweza kuiona idadi ya watu wasiohesabika waliokuwa uchi. Wote walijawa na wadudu waliowatambaa miili yao . Hakuna sehemu ya miili yao iliyosazwa kwani yote ilifunikwa kabisa na wadudu wale.

Wale watu wakiwa uchi walijaribu kuwafukuza wadudu wale huku wakisaga meno. Nikauliza , “ni nini walichokifanya watu hawa walipoishi duniani?”.



Hawa ni wale walioshutumiana na kusengenyana, hawakujali yale waliyoambiana. (Mathayo 5:22) niliwaona mapepo wakizidunga na kuzitoboa tumbo za watu wale wakitumia mundu. Singeweza kuzistahimili kelele zao. Nikawauliza malaika, “ni nini walichofanya watu hawa walipokuwa duiniani?”

“watu hawa walikuwa na kazi, majumba na hata jamii, lakini hawakumtolea Bwana Mungu. Hawakuwasaidia masikini, makanisa yao au kazi za Mungu, walikuwa wabanifu tena walafi. Hata walipokutana na masikini waliwapuuza na hawakuwajali. Walijali tu masilahi yao na ya jamii zao. Walivaa vizuri na kula vizuri na walikua na maisha ya starehe. Hii ndio sababu tumbo zao zinatobolewa kwani tumbo zao zilijaa tama”. ( methali 28:27)

Lilikuwa ni jambo la kuogofya sana. Baada ya kushuhudia jambo hilo, niliporudi duniani, nilipeana pesa na mali yangu yote kwa watu wengine. Wokovu hauwezi patikana kwa pesa au mali. Ni kwa imani pekee. Jehanamu hakustahimiliki na ni pahali duni. Ni mahali pa mateso. Niliona pia watu amabao vichwa vyao vilikatwa kwa msumeno mkali sana. Nikamuuliza malaika, “ni nini walichokifanya watu hawa? Ili wastahili mateso namna hii?”



Naye akanijibu, “ Mungu aliwapa akili ili wawaze mambo yaliyo mema tena yenya manufaa. Lakini hawa watu walikuwa na mafikira potovu tena machafu. Walifikiri kuhusu mambo ya tama na anasa”. (Mathayo 5:28)

Kish nikawaona watu wanadungwa na kukatwa vipande vipande. Ilitisha sana. Nikauliza “vipi kuhusu watu hawa? walifanya nini?, Hata wateswe nama namna hii?.” Malaika akaibu “hawa walikuwa mashemasi na wazee wa kanisa ambao hawakuzitumikia kanisa zao. Hawakutaka wala kupenda kuzitumikia kanisa zao wala kuzifanyia kazi. Wao walipenda tu kupokea na kupokea vitu kutoka kwa washirika wa kanisa”.

(Zecheria 11:17, hosea 6:5)

Nliwaona wazee wa kanisa ,mashemasi na waumini wa kawaida wakiteswa na mapepo. Mapepo yalitengeneza shimo katika ndimi zao na kuingiza kamba kupitia matundu yale kwenye ndimi zao. Kisha mapepo yakawaburura kwa kamba ile. Nikauliza tena. "walifanya nini duniani?" malaika akajibu, "wao walifanya dhambi nne tofauti. Kwanza waliwashutumu wachungaji wao. Waliongea mabaya kuwahusu. Waliwasengenya na kuwakejeli wachungaji wao." ()akobo3:6)( mathayo 12:37)



Nawasihi nyote mliofanya matendo kama haya tubuni! Tubuni!

Malaika akaendelea , "pili waliwasumbua wakristo wengine hadi hata wale waliokuwa waaminifu wakaathirika na kuacha kuja kanisani na hata wengine waliacha kuamini. Walifanya kila wawezavyo kuwafanya wakrsisto waaminifu wasitende kazi ya Bwana. Waovu hawa walisababisha waumni wengi wajikwae . mwisho kuna wake na waume waliokunywa pombe na kuwatusi watu wa jamii zao. Niliona mapepo wakitoboa tumbo za waume na wake wale kutumia msumari mkubwa. Niakuliza , " walifanya nini hawa? Malaika akanijibu . " hawa ni waume na wake walioishi pamoja pasina kuoana pia wana hatia ya uavyaji mimba kwani waliwahi kushika mimba pia na hawajatubu.".



Nikaoana kundi la watu. Mapepo waliikata midomo yao kama vile mtu akatavyo nyama au mboga kwa vipande vidogo. Niakuliza, "mbona watu hawa wanateswa hivi? Malaika akajibu, " hawa ni wana na mabinti , na mabinti na wana katika sheria waliojibizana na wazazia wao. Kile iliwapasa kufanya ni kuomba msamaha badala ya kufanya mambo kuwa mabaya zaidi. Wengi wao walitumia lugha ya matusi, waliwashambulia wazazi wao mananeo makali.waliasi. hii ndio sababu midomo yao inakatwa viapande vidogo."

Wandugu, sote tutakufa siku moja, lakini hatujui itakuwa lini. Tafadhali sameheaneni kila wakati na ipasavyo ikibidi. Tubu na utubu tena na fanya hivi hata siku nzima ikikubidi.

Wandugu wapendwa nilizipuuza shuhuda kama hizi . nilikuwa mchungaji wa kiprisbiteriani wa kihifadhina aliyepuuza mambo kama haya. Lakini sasa lazima niwashuhudie yale niliyo yaona.

Tafadhali usisite kuishi maisha matakatifu. Tafadhali epuka hukumu hii iliyojaa mateso mengi. Usiishi kwa ajili ya mwili wako bali jiwasilishe kwa ufalme wa Mungu. Tafadhali waombee wasiomjua Yesu. Waenezee watu injili na uzae matunda ya kiroho .Tafadhali omba asubihi sana na ifanye jumapili kuwa takatifu. Toa zaka ipasavyo. Jilimbikizie  tuzo mbinguni na sio humu ulimwenguni. Naomba na kukubariki kwa jina takatifu la Yesu.




Kutoka kwa mchungaji Park Yong Gyu.